1.0 UTANGULIZI



Parokia ya Bikira Maria mama wa Huruma mjimpya -relini Ipo Majohe Mjimpya kuvuka Reli ya Tazara . inapakana na Reli ya Tazara upande wa Kusini na kaskazini inapakana na bomba la gas la Songosogo upande wa Mashariki inapakana na barabara ya Gongo la mboto Mwera Rada, upande wa Magharibi inapakana na makutano ya reli na Bomba la Gas ya Songosongo. Tumezungukwa na majirani (yaani wakazi).

Eneo la Mjimpya Relini lilianza kukaliwa na wakazi wenyeji kwa wingi miaka ya 1990 na kufikia miaka ya 1995 idadi ya wakazi wa Mjimpya Relini iliongezeka . Kwa sababu ya kuongezeka kwa watu, haja ya kupata huduma mbalimbali za kijamii ilijitokeza mojawapo ya hizo ikiwa ni huduma za kiroho.

Eneo hili lilikuwa na Jumuiya moja ya Mashahidi wa Uganda Parokia ya Mt Agustino Ukonga Kutokanana umbali mrefu kutoka Jumuiya kwenda parokiani ilionekana waamini wengi walikuwa hawasali siku za jumapili. Ndipo viongozi waliokuwepo walipopata wazo la kutafuta na kununua eneo la kusalia na kumshirikisha baba Paroko wa Parokia ya Ukonga. wakati huo alikuwa Padri Lucas Kidegu.

Wafuatao ndio walikuwa viongozi wa Jumuiya ya Mashhidi wa Uganda wakati

1. Fredy Nshunju

2. Tito Makwela
3. Anastazia Manyanda
4. Jane Tarimo
5. Emilia T. Makwela

UNUNUZI WA ENEO

Mnamo mwaka 1998 Baba paroko alipeleka ombi kwa kwa baba Askofu mkuu wa Jimbo kuu la Dar es salaam . la kununuliwa Eneo na kueleza umbali uliopo kutoka jumuiya mpaka Parokiani.

Baba Askofu alidhiria kununua eneo na mwaka huo huo eneo lilinuliwa lenye Ukubwa wa Eneo la Ekari tatu.

KUANZA KUTUMIA ENEO KWA IBADA

Mwaka 2000 aliyekuwa Paroko wa Parokia Ukonga FR. Lucas Kidegu alihamishwa na Paroko Mpya Fr. Steven Nyailawila aliteuliwa kuwa paroko waparokia Ukonga.

Wakati Huo Jmuiya ya mashahidi wa Uganda ulikuwa imegawanywa na kupata Jumuiya ya Mt Krian Askofu na Mathia Mtume.

Mmnano tarehe ……..mwaka 2000 katika sikukuu ya Mathias Mtume misa ya kwanza ilisomwa katika eneo hilo na baba Paroko fr. Steven Nyilawila.

UJENZI WA BANDA LA KUSALIA

Mwaka 2004 Waamini waliokuwepo waliokuwepo alishirikiana na ku'goa visiki na kuanza kusali chini mikoroko . msalaba wa jubilee ya 2000 nao walikesha nao pale kwenye eneo na kupanda mti wa Jubilie .

Mwaka 2004- baba paroko wa Ukonga Fr Steven Nyilawila alipatanga kuwa ni Kigango cha Tazara Relini

Wafuatao ndio walikuwa Viongozi ndio Viongozi wa kwanza wa Kigango.

- Alfred Owino-mwenyekiti
- Pregrinus Chaula
- Sixtus Otieno
- Veronica Nyabumela
- Yustina Kibena

Viongozi hawa wakishirikiana na kamati ya Ujenzi waliweza kuhamasisha waamini na kupata fedha za kujenga banda la kusalia. Mwaka mwaka 2006 tulisha kuwa na banda la kusali na waamini walikuwa wanakaa kwenye matofali.

Viongozi wa kamati ya Ujenzi walikuwa ni.

- Raphael Bokango.
- Castro Ndungulu.
- Christopher Bamanyisa.
- Fredy Nshunju.

Kamati ikisaidiana na kamati tendaji waliweza kujenga kanisa la muda.

WATOA HUDUMA KWA KIPINDI HICHO

- Wakati tukiwa kigango tulikuwa na tunapatiwa huduma za kiroko kutoka parokia ya Ukonga lakini lazi kutoka kwa Fr. George Ndambala kutoka shirika la wapalotine.
- Pia mapadri kutoka katika seminari yaetu kuu ya segerea walikuwa wakisaidia kutupatia huduma za kiroho.
- Namano mwaka 2007 baba Askofu alitupatia Padri mkazi Fr. Sunny Mattahial wa shirika la Fransis De Sales ili awa mlezi wa Kigango chetu.
- Padre huyu aliaanza kukaa nyumba ya kupanga iliyop karibu na kanisa

IDADI ZA JUMUIYA WAKATI TUNAANZA KIGANGO

Wakati tunatangazwa kigango tulikuwa na Jumuiya Nnne

- Mashahidi wa Uganga
- Krian Askofu
- Mathias Mtume
- Vicent waPaulo

WAZO LA KUWA PAROKIA

Mmano mwaka 2008 mwezi was aba baba Kardinal Pengo alikuja ku weka jiwe la msingi wa kanisa pamoja na kutoa Sakrament ya ekaristi alitangaza kigango cha Tazara relini kuwa parokia Teule na kumtangaza fr Sunny Mathathili kuwa padre mkazi

Mwaka huu huo mwezi wa tisa tulitangawa kuwa parokia ya Bikira Maria mama wa Huruma Mjimpya Relini. Na FR Sunny Mathathili kuwa Paroko wa kwanza.



FR. SUNNY MATATHIL- MSFS- PAROKO WA KWANZA MJIMPYA RELINI .

Kamati tendaji ya kwanza walikuwa hawa wafuatao

1. EMMANUEL MALABA- MWENYEKITI
2. MOSES MAYA-MAKAMU MWENYEKITI
3. DATIVA SHOWE- KATIBU
4. DEUSDEDIT MAIGA-KATIBU MSAIDIZI
5. ABDOGAST MATATA- MWEKA HAZINA

AWAMU YA PILI

1. ALFRED OWINO-MWENYEKITI
2. ANTONY MENSON SHOWE- MAKAMU MWENYEKITI
3. DEUSEDEDIT MAIGA- KATIBU
4. PASCHAL MAZIKU- KATIBU MSAIDIZI
5. BEATRICE MASSAWE- MWEKA HAZINA

AWAMU YA TATU


1. ALFRED OWINO- MWENYEKITI
2. MOSES MAYA- MAKAMU MWENYEKITI
3. DATIVA SHOWE- KATIBU
4. NICKSON LUDOVICK – KATIBU MSAIDIZI
5. BEATRICE MASSAWE- MWEKA HAZINA



Katibu, mweka hazina na katibu msaidizi



Katibu, mweka hazina , mwenyekiti, paroko , mkuu wa shirika katibu msaidizi wa jimbo , katibu msaidiz na nyuma ni paroko msaidizi



PAROKO WA MJIMPYA RELINI

UJENZI WA KANISA LA KUDUMU

Mwaka 2008 ujenzi wa kanisa la Kudumu ulianza na kamati ya Ujenzi kwa kipindi hicho walikuwa wafuatao

- Amossy Itozya
- Laurent Kadiwa
- Mr Kalinga
- Fredy Nshunju
- Alfred Owino
- Theresia Cosmas

Na mpango ilikuwa ni kupata kanisa kubwa la kudumu na Jiwe la msingi liliwekwa na Polcapo cardinal Pengo mwaka 2018

UJENZI WA NYUMBA YA MAPDRI

Mnamo mwaka 2010 Tulianza tulianza ujenzi wa nyumba ya padre jiwe na msingi liliwekwa na mhashamu askofu msaidizi wa Jimbo kuu la Dar es salaam mwaka 2010

Nyumba hiyo ya gorofa moja ilifunguliwa na kubarikiwa Askofu mkuu wa Jimbo kuu la Dar es salaam Polcarpo cardinal Pengo. mwaka 2012

Pia siku hiyo pia alitoa upadrisho kwa Kwa padre INNOCENT NGOWI-MSFS



Hapa ni ujenzi wa kanisa ukiendelea, Kanisa ambalo lipo mpaka sasas





KUBARIKI KANISA NA KUTABARUKU ALTARE

Mnano tarehe …08 mwezi 10 mwaka 2011 Baba Kardinal alikuja kutabaruku altare na kubariki kanisa jipya. Pia siku hiyo alitoa sakrament ya Kipaimara kwa vijana Zaidi ya 150



NYUMBA YA MAPDRI – MJIMPYA RELINI

VIGANGO VYA PAROKIA YETU

Parokia yetu ya Mjimpya relini ina vigango vitano .

1. Kigango cha Mtakatifu Mathias Mtume
2. Kigango cha mtakatifu Thomas waAkwino
3. Kigango cha Bikira Maria wa Rozari
4. Kigango cha Mt Theresia wa Mtoto Yesu
5. Parokia Teule ya Mt Anton wa Padua

KIGANGO CHA MT MATHIAS MTUME

Kigango hiki ndio kipo makao makuu ya parokia na kina Jumuiya 50 na kanda 11.

Kigango kinapakana na parokia ya Ukonga, parokia ya Pugu , Kigango cha Thresia wa mtoto YeSU Rada , Kigango cha BOMBA MBILI NA kIGANGO CHA Mt THOMAS WA aKWINO.

Katika kigango hiki kuna vyama vya kitume vifuatavyo

- UWAKA
- WAWATA
- VIJANA
- LEOGIO MARIA
- UTOTO MTAKATIFU
- KARISMATIKI KATOLIKI

- MOYO MTAKATIFU WA YESU
- UKWAKATA
- YUSUPH ALMATEA

KIGANGO CHA MT THOMAS WA AKWINO

Eneo la kigango hiki lilinunuliwa mwaka 2010.kwa pesa ya mkopo tuliyopatiwa na baba cardinal Pengo.

Kigango kilizinduliwa rasmi na aliyekuwa paroko wa Mjimpya kipindi hicho Fr. Sunny Mathathil. mwaka 2011

Kigango hiki kipo maeneo ya kipunguni B Machimbo.kina pakana na Parokia ya Ukonga na Parokia ya Kitunda na Kigango cha Mathias Mtume

Kigango hiki kina Jumuiya 17 na kanda 4.

Manamo mwaka 201.walianza ujenzi wa nyumba wa mapdri amabyo kwa sasa inatumika kama ofisi ya padri walei na katekista .

Jiwe la msingi la nyumba hiyo uliweka na Askofu wa Ifakara Salutaris Libena mwaka 2016 na mwaka 2019 Askofu mkuu wa Jimbo kuu la Dar es salaam Thadeus Rwai'chi alizindua nyumba hiyo na kubariki.

KIGANGO CHA BIKIRA MARIA WA ROZARI

Kigango hilki kilianzishwa mwaka …kabla ya kigango cha Tazara Relkini ambacho sasa ni Parokia ya Mjimpya

na kigango kikongwe kuliko vyote.

Kigango hiki kipo maeneo ya bomba mbili ni kilometer 9 kutoka parokiani.

Kigango hiki kina jumuiya 22 na kanda 6

Kigango hiki kinapakana na parokia ya Kitunda na kigango cha Mathias Mtume, kigango cha Theresia wa Mtoto Yesu , parokia Teule Chakenge.

- Kigango cha Bikira Maria mama wa Rozari kimeanza ujenzi wa nyumba ya padri na kupanua kanisa lao.
- Pia katika kigango hiki kuna vyama vya Kitume kama vifuatavyo
    1. UWAKA
    2. WAWATA
    3. VIJANA
    4. UTOTO MTAKATIFU
    5. UKWAKATA
    6. KARISMATIKI KATOLIKI
    7. LEOGIO MARIA
    8. WATUMISHI WA ALTARE
    9. MOYO MTAKATIFU WA YESU

KIGANGO CHA THERESIA WA MTOTO YESU

Mwaka 2010 waamini wa maeno haya walianza kusalia katika majengo ya Chuo cha Ualimu Rada.

Mnamo mwaka 2011. Mapdri wa shirika la Litte Flowers walinunua eneo huku Rada na kutupatia nusu Hekari kwa ajili ya kujengea kanisa. Lakini baada ya mwaka mmoja waliamua kuliuza hilo eneo lote na Kanisa lilinunua kiwanja Eneo hili yenye ukubwa wa Hekari tano na kujenga banda la kusalia la muda

Mwaka 2012 aliyekuwa paroko wa Mjimpya Fr. Sunny Mathathi alitangaza Rada kuwa Kigango cha mt Theresia wa mtoto Yesu.

Kigango hiki kina Jumuiya 18 na kanda 5.

Kigango hiki kinapakana na kigango cha Mathias Mtume , Kigango cha Bombambili , Parokia Ya Puguna Parokia ya Chanika.

Kigango Hiki kina vyama vya Kitume vifuatavyo

1. UWAKA
2. WAWATA
3. VIJANA
4. UTOTO MTAKATIFU
5. KARISMATIKI KATOLIKI
6. WATUMISHI WA ALTARE

PAROKIA TEULE ANTON WA PADUA CHAKENGE

Mnamo mwaka 2008 muumini moja alijitolea eneo lake ili kiwe kituo cha sala eneo hilo lilikuwa na ukumbwa kwa 20 kwa 20.

Ndipo lilijengwa banda la makuti kusalia.

Mnamo mwaka 2009 Aliyekuwa paroko wa parokia ya Mjimpya Relini Fr. Sunny Mathathil aliomba mkopo Jimboni na kununua eneo la Ekari nne ambapo ndio lilipojengwa kanisa nyumba ya katekista na nyumba ya Mapadri.

Mnamo mwaka 2013 aliyekuwa askofu saidizi wa jimbo kuu la Dar es salamm Titus Mdoe alibariki kanisa

Na mnamo mwaka 2014 jiwe la msingi la nyumba ya Mapdri liliwekwa na Askofu Kuuu wa Jimbo kuu la Dar es salaam Policapo cardinal Pengo.

UHAI WA VYAMA VYA KITUME.

UWAKA

Utume wa Wanaume Katoliki ni Chama cha Kitume chenye wanachama wa kutosha katika Parokia yetu.

Wamekuwa wakishiriki shughuli mbalimbali za Kitume ndani na nje ya parokia yetu.

wamekuwa wakijitolea kuwalea wadada wadogo.

WAWATA

Wanawaka wakatoliki Tanzania ni chama cha kitume kinachowaunganisha wanawake wote wakatoliki.

Wamekuwa wakifanya utume mbalimbali katika parokia yetu ikiwa ni pamoja na kufanya matendo ya Huruma ndani nan je ya Parokia

Wamekuwa wakiwalea vijana wa Novishieti ya Francisco de Sales Mkuza .

Wamekuwa wakishiriki na wanawake wengine wa Jimbo kuu la Dar es salaam katika kuwategemeneza waseminary wa Voisiga

Wamekuwa wakiangalia mahitaji ya nyumba ya mapadri .

VIJANA

Hiki ni chama cha Kitume kinachowaunganisha vijana wote wanaosoma (TYSC) na wanaofanya kazi (VIWAWA).

Vijana hawa wamekuwa wakifanya utume wao ndanina nje ya parokia

Wamekuwa wakishirikiana na vijana wa decani na jimbo katika matamasha , michezo na matukio mbalimbali

UTOTO MTAKATIFU

Hiki ni chama kinachowaunganisha watoto wote wakatoliki .

Watoto hawa wamekuwa wakifanya utume wao wa uinjilishaji ndani nan je ya parokia yetu.

Wamekuwa wakishriki matukio mabalimbali pamoja na safari za kimisionari za Jimbo.

VYAMA/VIKUNDI VINGINE

Katika parokia yetu vyama vingine vimekuwa vikifanya Utume wao kwa mujibu wa katiba yao na utaratibu wa chama /kikundi husika

KAMATI TENDAJI YA SASA 2026

Michael Magubika
Alfred A. Mushi
Jeremiah Ladslaus
Charles Silayo
Rehema C. Bugomolo

MUNGU AWALINDE NA KUWABARIKI

